/

# HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA

## TAARIFA YA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA, JENGO LA MATIBABU YA DHARURA NA NYUMBA YA WATUMISHI KUPITIA FEDHA ZA UVIKO – 19 HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA

**UTANGULIZI:**

Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ilipokea fedha Sh. 1, 300,000,000.00 kwa ajili ya Ujenzi wa vyumba 65 vya Madarasa ya katika Shule 26 za sekondari, ikiwa ni utekelezaji mpango maendeleo wa ustawi wa Taifa na Mpango dhidi ya Uviko – 19. Halmashauri kupitia fedha hizo imejenga vyumba vya madarasa 65 katika shule 26 za Sekondari ambapo majengo yote yamekamilika na kuwekewa madawati 50 katika kila darasa na yanatumika. Ili kukabiliana na changamoto ya vyumba vya madarasa, Serikali kupitia fedha hizo imekamilisha madarasa hayo na sambamba na kuweka madawati kwa lengo la kuwaondolea changamoto ya kupata elimu inayogusa Elimu moja kwa moja.

Aidha Halmashauri ilipokea Sh. 390,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la matibabu ya dharura ambalo limetengewa Sh. 300,000,000.00 na Nyumba ya Watumishi ambayo imetengewa Sh. 90,000,000.00. Ujenzi wa jengo la matibabu ya dharura na nyumba ya Mtumishi ya 2in 1 mbili unaendelea na utakamilika ifikapo tarehe 22/06/2022.

Katika utekelezaji wa ujenzi wa vyumba vya madarasa, ujenzi wa jengo la Matibabu ya Dharura na Nyumba ya Mtumishi 2in 1 mbili, Halmashauri ilifanya mambo yafuatayo:-

1. Kuunda kamati za ufatiliaji ngazi ya Wilaya ambayo ilijumuisha watumishi 9 kama ifuatavyo:-
    i. Mkuu wa Wilaya - Mwenyekiti
    ii. Mkurugenzi Mtendaji Wilaya – Katibu
    iii. Mweka Hazina wa Halmashauri – Mjumbe
    iv. Afisa Mipango – Mjumbe
    v. Afisa Elimu Sekondari – Mjumbe
    vi. Mhandisi wa Ujenzi Wilaya – Mjumbe
    vii. Afisa Maendeleo ya Jamii – Mjumbe
    viii. Afisa Manunuzi – Mjumbe

Scanned with CamScanner

ix. Mganga Mkuu wa Halmashauri – Mjumbe

2. Kuandaa makadirio ya mhandisi ya Vifaa vyote vya Ujenzi wa Madarasa 65, Jengo la Matibabu ya Dharura (EMD) na Nyumba ya Mtumishi ya 2in 1 (Nyumba 2)
3. Kubainisha utaratibu wa Force Account kutumika kwenye ujenzi wa majengo tajwa hapo juu.
4. Kufanya uchambuzi wa kuwapata mafundi wazoefu wenye uwezo wa kufanya kazi nzuri na kuleta thamani ya fedha

Hadi kufikia tarehe 09/06/2022 ujenzi wa vyumba vya madarasa ulikuwa umekamilika na Mdarasa yote 65 yanatumika. Aidha Ujenzi wa jengo la matibabu ya dharura na nyumba ya Mtumishi ya 2in 1 (nyumba 2) unaendelea na ujenzi utakamilika ifikapo tarehe 22/06/2022.

Naomba kuwasilisha,

Nice R. Munissy
**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA**
**HALMASHAURI YA WILAYA**
**SHINYANGA**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
S.L.P. 93
SHINYANGA

Scanned with CamScanner

**KIAMBATANISHO**

## ORODHA YA SHULE 26 ZA SEKONDARI ZILIZOPEWA FEDHA ZA UVIKO-19

| Na. | Jina la Shule | Idadi ya vyumba vya madarasa | Kiasi kilichopokelewa |
|---|---|---|---|
| 1 | Usanda sekondari | 3 | 60,000,000.00 |
| 2 | Shingita sekondari | 2 | 40,000,000.00 |
| 3 | Kituli sekondari | 2 | 40,000,000.00 |
| 4 | Solwa sekondari | 3 | 60,000,000.00 |
| 5 | Isela sekondari | 2 | 40,000,000.00 |
| 6 | Salawe sekondari | 3 | 60,000,000.00 |
| 7 | Pandagichiza sekondari | 2 | 40,000,000.00 |
| 8 | Itwangi sekondari | 3 | 60,000,000.00 |
| 9 | Mishepo sekondari | 2 | 40,000,000.00 |
| 10 | Tinde sekondari | 3 | 60,000,000.00 |
| 11 | Zunzuli sekondari | 2 | 40,000,000.00 |
| 12 | Gembe sekondari | 3 | 60,000,000.00 |
| 13 | Mwantini sekondari | 2 | 40,000,000.00 |
| 14 | Kaselya sekondari | 2 | 40,000,000.00 |
| 15 | Mwalukwa sekondari | 2 | 40,000,000.00 |
| 16 | Ng'wakitolyo sekondari | 3 | 60,000,000.00 |
| 17 | Masengwa sekondari | 2 | 40,000,000.00 |
| 18 | Ihugi sekondari | 3 | 60,000,000.00 |
| 19 | Lyabusalu sekondari | 3 | 60,000,000.00 |
| 20 | Lyabukande sekondari | 3 | 60,000,000.00 |
| 21 | Ilola sekondari | 3 | 60,000,000.00 |
| 22 | Imenya sekondari | 3 | 60,000,000.00 |

Scanned with CamScanner

| | | | |
|---|---|---|---|
| 23 | Iselamagazi sekondari | 2 | 40,000,000.00 |
| 24 | Imesela sekondari | 2 | 40,000,000.00 |
| 25 | Didia sekondari | 2 | 40,000,000.00 |
| 26 | Usule sekondari | 3 | 60,000,000.00 |
| Jumla kuu | | | 1,300,000,000.00 |

MIRADI YA AFYA ILIYOPEWA FEDHA ZA UVIKO-19

| Na. | Jina la mradi | Kiasi kilichopokelewa |
|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa jengo la matibabu ya dharura | 300,000,000.00 |
| 2 | Nyumba ya mtumishi 3in 1 | 90,000,000.00 |
| Jumla kuu | | 390,000,000.00 |

Scanned with CamScanner